

KUMBUKIZI YA WILHELM J. G. MÖHLIG

2/9/1934 – 6/8/2023

LUTZ DIEGNER



Picha imetumiwa kwa idhini ya familia ya Marehemu.

Yeyote aliyebahatika kusomeshwa naye atamkumbuka profesa ambaye alikuwa na ukwasi wa ujuzi, uwingi wa vipaji na ucheshi wa aina yake: Marehemu Profesa Wilhelm J. G. Möhlig. Mwaka uliopita wa 2023 mwezi wa nane tarehe sita, aliitwa na Mungu wake akapumzike mahala pema peponi. Jumuiya ya wasomi wa Masomo ya Afrika tunamwomboleza tukimkumbuka na kumshukuru kwa mchango wake mkubwa aliutoa kwa uwanja huu mzima. Mbali na fani yake haswa ya isimu ya lugha za Kiafrika, alichangia makubwa katika kukuza Masomo ya Afrika kwa ujumla wake, huku nchini Ujerumani, Ulaya nzima na Afrika.

Ulipomwuliza kumekuwaje kuwa ameingia katika uwanja huu alikujibu kwa utani uliosema ukweli: “Wajua nilikuwa tayari nimeshajifunza kazi nyingine mbili, mfanya biashara ya chuma – nikizitii nasaha za baba yangu – na mwanasheria!” Walakini, hakutosheka na kazi hizi mbili

KUMBUKIZI YA WILHELM J. G. MÖHLIG

akaamua kuendelea kusoma masomo mengine kabisa, masomo ya lugha za Kiafrika. Hata yeye mwenyewe asingalitarajia kuwa baadaye atakuwa profesa wa fani hiyo Chuo Kikuu cha Koloni, na hata baada ya kustaafu kuendelea na utafiti hadi siku zake za mwisho.

Wilhelm Johann Georg Möhlig alizaliwa tarehe pili mwezi wa tisa mwaka 1934 mjini Essen huku Ujerumani Magharibi, eneo la “Ruhrpott” (lakabu yenye maana ya “chungu kikubwa” kinachowajumuisha watu wengi maeneo ya mto Ruhr yenye viwanda vingi) lililo maarufu kwa wepesi wa watu kujuana, kuwasiliana na kutaniana katika maisha ya kila siku. Kama tulivyosimulia hapo juu, baba yake aliyekuwa mfanya biashara ya chuma alimtaka afuate nyayo zake akatii, lakini baadaye, akiwa na motisha ya kupata elimu ya juu zaidi, akaamua kusomea sheria. Walakini, kazi mbili hizo zilikuwa hazikumtoshia. Shemeji yake Jürgen Christoph Winter ambaye alisoma naye sheria na baadaye kuwa profesa wa Masomo ya Afrika ndiye aliyemshawishi akavutiwa na Masomo ya Afrika na hasa lugha zake. Marehemu aliyekuwa na kipaji cha ajabu cha lugha akaanza kusoma masomo hayo kwa furaha na bidii, na kuamua kuwa atapenda kujiendeleza hadi kiwango cha shahada ya tatu.

Hapo ndipo mwanzilishi wa Masomo ya Afrika hapo Chuo Kikuu cha Koloni, Oswin Köhler, alipomshauri Marehemu afanye utafiti huko kaskazini mashariki ya Namibia ya leo, ukanda ambao umeitwa wa Caprivi. Mwaka 1965 ndipo alipokwenda kufanya utafiti huko yaani kutafiti lugha ya Kigciriku, mojawapo ya lugha za Kibantu za eneo hilo, maarufu kwa kuwa na baadhi ya sauti mahsuszi za lugha za Kikhoisan. Kazi hii aliichapisha kama tasnifu yake ya shahada ya tatu mwaka 1967, na hata miaka thelathini baadaye, akarudi huko Namibia pamoja na wanafunzi wake wakaendelea na utafiti wa lugha hii na lugha nyingine za jirani.

Ndivyo alivyoingia katika masomo ya lugha za Kibantu ambayo yalimpeleka Afrika Mashariki pia. Miaka ya 1969-1972 alifanya utafiti wa lugha na lahaja za mlimani Kenya uliozaa tunda la kitabu kilichochapishwa mwaka 1974. Miaka ya 1973-1975 alisomesha na kufanya utafiti Chuo Kikuu cha Nairobi na kuwashuhudia wasomi na waandishi maarufu Okot p’Bitek na Ngugi wa Thiong’o akifanya kazi nao ‘mlango wa pili’. Licha ya kuwa mwanasheria na mwanaisimu, alikuwa amevutiwa sana na fasihi simulizi na vilevile fasihi andishi za Afrika.

Baada ya wakati wake huko Nairobi, pamoja na mtafiti mwenzake Bernd Heine, alichapisha kitabu juu ya lugha na lahaja za Kenya nzima kilichotoka mwaka 1980, mwaka ule ule alipopewa upofesa wa lugha za Kiafrika huku Chuo Kikuu cha Koloni. Mwaka 1984/1985 alichapisha makala tajika kuhusu lahaja za Kiswahili za Kenya akizilinganisha na lugha za Kimijikenda na za bonde la mto wa Tana. Kazi nyingine kuu ya utafiti wake huko Kenya inayochunguza lugha na lahaja za pwani ya Kenya ilichukua muda mrefu sana kufinyangwa hatimaye ikachapishwa mwaka 2022, miezi michache tu kabla hajafariki. Katika uwanja wa utafiti wa lugha za Kibantu, Marehemu alikuwa amejenga sifa yake tajika kitaifa na kimataifa.

KUMBUKIZI YA WILHELM J. G. MÖHLIG

Mbali na shughuli zake hizo za utafiti, Marehemu pia alikuwa uwanja wa masomo ya sheria ya Afrika, na masomo ya Afrika kwa ujumla. Alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa Jumuiya ya Masomo ya Afrika ya Ujerumani mwaka 1969 na wa Shirika la Sheria ya Afrika ya Ujerumani mwaka 1973. Mwaka 1988 akishirikiana na Profesa Bernd Heine alimshawishi Rüdiger Köppe akaanzishe shirika la uchapishaji lenye jina lake, Rüdiger Köppe Verlag, ambayo hadi leo imetoa kazi takriban mia tisa zihusuzo nyanja zote za Masomo ya Afrika, hasa za lugha za Kiafrika na utafiti wa kiisimu. *Tulipohariri muswada wa kumbukizi hii, tumepata habari ya kusikitisha sana kuwa naye Rüdiger Köppe aliyekuwa na miaka 62 tu ameaga dunia tarehe 15 mwezi wa sita mwaka 2024. Jumuiya ya wasomi wa Masomo ya Afrika hatuna budi tumshukuru kwa kazi yake kubwa na isiyo na kifani ya kuchapisha uwingi wa ajabu wa vitabu vya masomo yetu haya. Mungu amlaze mahali pema peponi!*

Tukimkumbuka Marehemu Wilhelm Möhlig, tusingahau pia kuwa alikuwa mpenzi mkubwa wa lugha ya Kiswahili. Yeye na mwenzake Bernd Heine waliandika kitabu cha kufundishia Kiswahili kwa lugha ya Kijerumani, kitabu kilichochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1968 na kufinyangwa na kutolewa tena mara kadhaa hadi mwaka 1999 kikawa kitabu cha kiada kwa miongo mitatu na zaidi. Vilevile alisaidia sana kuenzi na kukuza ufundishaji wa Kiswahili siyo chuoni kwake tu, bali pia vyaonzi pengine Ujerumani, Austria na Uswisi. Kwa upande wa utafiti, hakukosa kuhudhuria ‘Swahili Colloquium’, Kongamano la Kiswahili la kila baada ya miaka miwili, na la kila mwaka baadaye, lililoanzishwa na Gudrun Miehe, aliyekuwa profesa wa Masomo ya Afrika wa Chuo Kikuu cha Bayreuth. Pamoja naye alihariri kitabu chelezi cha Kiswahili kwa lugha ya Kijerumani walipowajumuisha watafiti watajika wa kongamano hilo.

Wanafunzi wake Marehemu Thomas Geider, gwiji wa fasihi simulizi za Afrika, na Rose Marie Beck, aliyekuwa profesa wa Masomo ya Afrika Chuo Kikuu cha Leipzig, pamoja na Werner Graebner, gwiji na mwanaharakati wa fani mbalimbali za muziki wa Afrika Mashariki, walipoanzisha jarida letu la *Swahili Forum*, awali likiwa ni toleo maalumu la *Afrikanistische Arbeitspapiere* (AAP), aliwatia moyo na kuwaunga mkono katika jitihada zao za kulichapisha jarida hilo chuoni Koloni kabla halijahamia Mainz, kugeuzwa jarida la mkondoni na kuhamia Leipzig baadaye.

Kuvutiwa kwake na fasihi kumeshatajwa hapo juu. Karibu kumemtoa uhai wake mapema! Ndivyo alivyozoea kusema akisimulia kisa na mkasa wa kutafsiri magnum opus (kazi kuu) ya Aniceti Kitereza, Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. Ntulanalwo na Bulihwali (1980) kwa lugha ya Kijerumani. Mara baada ya kuhitimisha muswada wa tafsiri hii ambayo ilichapishwa mwaka 1990 na 1991 kwa jina la *Die Kinder der Regenmacher* (‘Watoto wa Waganga wa Mvua’) alikwenda kutembea msituni kwa nia ya kulegeza mwili na akili akapata kiarusi. Mungu wake alimpenda yaani alipata nafuu baada ya kupewa matibabu yaliyokuwa mapya wakati ule.

KUMBUKIZI YA WILHELM J. G. MÖHLIG

Mbali na kazi hiyo ya kutafsiri, alivutiwa sana na fasihi simulizi za Afrika akakuza utafiti wa uwanja huu ambapo walibobea wanafunzi wake kadhaa kama Marehemu Thomas Geider na mhariri mwenzetu Uta Reuster-Jahn. Mimi mwenyewe pia nilifurahi sana kuwa alikuwa amepokea kwa mikono miwili nia yangu thabiti ya kufanya utafiti wa fasihi ya kisasa ya Kiswahili.

Mbali na sheria, isimu na fasihi, pia hatuna budi tutaje kuvutiwa kwake na historia maana mbali na kuunganisha mada za kiisimu na za kihistoria, pia alihakikisha kwamba historia ya Afrika, hasa ya kabla ya ukoloni, ilikuwa inafundishwa katika Chuo Kikuu cha Koloni kila muhula, na yeye mwenyewe aliwajibika kulitekeleza hilo. Hayo yote yanaonyesha kuwa Marehemu alikuwa mtaalamu wa mambo mengi akifanana na wataalamu wa zamani walioitwa Universalgelehrte (wasomi wa mambo yote). Hakutosheka na fani moja au mbili, na daima alikuwa tayari kujifunza na kufundisha mapya na kukaribisha fani nyingine.

Bila ya shaka kumekuwa na kazi na sifa zake muhimu ambazo ninashindwa kuzifahamu na kuzitaja zote hapa. Walakini, nahisi kuwa sifa yake mojawapo, mbali na upana wa nyanja alizozitafiti na kuzifundisha, na ukarimu wake wa kukaribisha nyanja nyingine tena na kuwasaidia wanafunzi wake kujiendeleza, itakumbukwa sana na wengi waliomfahamu. Sifa hiyo ni ucheshi wake, ucheshi wa kutumia weledi wa kipaji chake cha lugha, ucheshi wa kutumia kejeli na tashtiti, ucheshi wa ‘kusoma hali’ na ‘kusoma watu’, na ucheshi wa kupenda kucheka na wenzake. Ucheshi huu unaonekana wazi ukisoma kitabu chake cha kitawasifu kilichochapishwa mwaka 2018 anaposimulia hasa wakati wake wa kufanya utafiti Namibia mwaka 1965. Ni ucheshi ule ule tulioufaidikia sisi wanafunzi wake tulipokwenda kushauriwa naye. Hata kama wakati mwingine nasaha zake za kitaaluma zilikuwa kali kidogo, hakukosa kumchekesha yeyote aliyeongea naye kwa utani wa aina yake.

Sasa tukiwa tunamkumbuka, tukisoma maandishi yake, hasa yale ya kitawasifu, tunahisi bado yuko nasi, tukimsikiliza, tukizungumza naye. Tukinena “Shikamoo Profesa!” atafurahi kusalimiwa kwa lugha ya Kiswahili na kutabasamu. Na muda si mrefu tukizungumza naye, kicheko chake cha kipekee kitasikika.

Kwa hakika, hatasahaulika kamwe!

Marejeleo / Kazi teule za Marehemu Wilhelm J. G. Möhlig

1967. *Die Sprache der Dciriku*. Hochschulschrift, Universität zu Köln.

1968 (pamoja na Bernd Heine). *Grundkursus des Swahili für den Unterricht im Sprachlabor*. Bad Honnef: Deutsche Stiftung für Entwicklungsländer.

1974. *Die Stellung der Bergdialekte im Osten des Mount Kenya*. Berlin: Reimer.

KUMBUKIZI YA WILHELM J. G. MÖHLIG

1980. (pamoja na Bernd Heine). *Language and Dialect Atlas of Kenya*. Berlin: Reimer.
1994. Kitabu cha heshima ya siku ya kuzaliwa ya kutimiza miaka sitini: Geider, Thomas & Raimund Kastenholz (Wahar.). 1994. *Sprachen und Sprachzeugnisse in Afrika*. Eine Sammlung philologischer Beiträge, Wilhelm J.G. Möhlig zum 60. Geburtstag zugeeignet. Köln: Köppe.
- 1995 (kuhaririwa na Gudrun Mieke). *Swahili-Handbuch*. (*Afrikawissenschaftliche Lehrbücher* 7). Köln: Köppe.
- ⁴1999. [¹1991]. *Swahili Grundkurs*. (*Afrikawissenschaftliche Lehrbücher* 3). Köln: Köppe.
2018. *Trommeln in der Kirche: Als Sprachforscher unter den Bantu-Völkern am Nordrand der Kalahari*. Köln: Köppe.
2022. *The Bantu Languages of the Kenya Coast: Aspects of Comparison and Contact*. Köln: Köppe.